

TANGAZO LA SERIKALI Na..... 788 la tarehe 30 SEPTEMBER, 2011

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
CHAPITO KATIKA GAZETI LA

(SURA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(2) wa 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO, 2010 ZA MWAKA 2011

lina na mwanzo wa kutumika 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro za mwaka 2010 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

eneo la matumizi 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:

“Ada” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

“Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“Plinth area” maana yake ni eneo la jengo liliotumika kujenga.

“Sheria” maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290.

“Taka” kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kiminiwa, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazi, uozo au hali uyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira ambayo inajumuisha taka.

“Taka nguzuu” maana yake ni taka ambazo lazika katika umajimaji kutoka majambani. Katika majengo ya biashara, vuwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyaonia, karatasi plastic au taka laini

